**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA SEKONDARI**

**MTIHANI WA KIDATO CHA KWANZA**
**KISWAHILI**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA MEI 2024**

---

## SEHEMU A (Alama 15)

**1. @1Alama 1=Alama 10**

| SWALI | i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JIBU | E | C | B | D | C | C | D | A | B | B |

**2. @1Alama 01=Alama 05**

| Orodha A | i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | D | G | A | C | E |

## SEHEMU B (Alama 70)

**3.** Mwanafunzi anatakiwa atunge sentensi tano tofauti zenye viunganishi vya sababu ;- **ALAMA 10% @2**

i. Lukwaro alilia **kwa sababu** alichapwa.
ii. Yeye alifaulu **kwa kuwa** alisoma.
iii. Asha aliwahi **ili** asichelewe basi
iv. Liandeli alipiga kelele **kusudi** asaidiwe
v. Mwinjuma alikasirika **kwa vile** alibiwa pesa zake

4. Mwanafunzi anatakiwa aelezee mambo Matano ya kuzingatia wakati wa kufasiri maana ya lugha **Alama 10@2**

i. Mfumo
ii. Sauti
iii. Nasibu
iv. Maana
v. Mawasiliano
vi. Kukubaliwa na binadamu

5. Mwanafunzi anatakiwa aelezee faida za picha na michoro kwenye kamusi **ALAMA 2% jumla 10%**

i. Huwezesha watumiaji wa kamusi kuundaa dhana ya jambo,hasa kama ni geni
ii. Huvuta umakini wa mtumiaji kamusi na kumfanya azingatie anachotazama.
iii. Huwasaidia watumiaji wa kamusi kutofautisha vitu vinavyokaribiana kimaana au kimaumbile.
iv. Huwawezesha watumiaji wa kamusi kuona mfanano baina ya vitu.
v. Maumbo hunata katika kumbukumbu za watumiaji na kuwawezesha kukumbuka maana kwa urahisi.
vi. Huifanya kamusi ivutie , hasa zinapotumia rangi.

6. Mwanafunzi anatakiwa ajue ataje vipera vinne vya fasihi simulizi alivyoviona **ALAMA 2% jumla 10%**

i. SOGA
ii. MAGHANI
iii. MIZUNGU

iv. MIVIGA
v. TARIHI

7. Mwanafunzi anatakiwa afafanue istilahi alizopewa ALAMA **2% jumla 10%**
   a) Wakaa Ni muda unatumika kutamka sauti za lugha
   b) Shadda Ni mkazo au nguvu inayutumika kutamka baadhi ya silabi za lugha
   c) Kidatu Ni kiwango cha sauti kinachosikika wakati wa mazungumzo
   d) Kiimbo Ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa uzungumzaji
   e) Fonimu Ni sauti za lugha mahususi zenye maana.

8. Mwanafunzi anatakiwa afafanue mambo Matano yanayotofautisha fasihi na matawi mengine ya sanaa.**ALAMA 2% jumla 10%**
   i. MUUNDO
   ii. MTINDO
   iii. LUGHA
   iv. WAHUSIKA
   v. MANDHARI

9. Majibu kulingana na habari;

a) Maana ya maneno : alama **05 @ 1**

i. **Kamati** ni kikundi cha watu waliochaguliwa kutokana na kundi kubwa la watu ili kushughulikia kazi au jambo fulani
ii. **Sudi ni** bahati
iii. **Inda** ni kuwa na wivu au husuda
iv. **Hamasa** ni hamu au uwezo wa kufanya jambo kwa bidii
v. **Sera** ni mikakati, au mongozo au mipango mbalimbali

(b) Kichwa cha habari ni USANIFISHAJI WA KISWAHILI **(Alama 01)**

(c) Usemi Mungu hamtupi mja wake unamaanisha kila mtu ana riziki yake kutoka kwa mwenyezi Mungu**.** **(alama 01)**

(d) kufupisha kwa maneno 60. **(Alama 03)**

- Mtahiniwa asome habari yote mpaka aielewe.
- Achague taarifa na maneno muhimu tu (abaini mawazomakuu tu)
- Katika ufupisho wake mtahiniwa azingatie wazo kuu la habari

**SEHEMU C: (Alama 15)**

10. Mwanafunzi anatakiwa aandike barua ya kirafiki kwa kuzingatia mambo yafuatayo: -

**ANWANI YA MWANDISHI**

**TAREHE**

**MWANZO WA BARUA**

**SALAMU**

# KIINI CHA BARUA

**MWISHO WA BARUA**

**JINA LA MWANDISHI**